



Jina langu ni Shyam, nina miaka kumi.
Mimi ni mwembamba, lakini mjasiri!
kuamuka mapema asubuhi kuenda shule sio furaha kamwe
bado huwa ninahisi usingizi niamkapo, nahisi naweza anguka.



Huwa bado nimefunga macho ninapo anza kusugua meno,
Nina msikia Amma akitengeneza samosa kwa haraka.
Akili zangu huanza kuwaza mbali,
Na mawazo mengi hunijia .



Je ingelikuwa aje kama shingo langu lingekuwa mara kumi urefu?
Nusu ningekuwa shuleni, nusu ningekuwa nyumbani, ningekuwa wapi?



Je ingelikuwa aje kama miguu zangu zingekuwa mrefu kama miti?
Mjengo wa shule yangu ungenifikia kwa magoti tu!



Je ingelikuwa aje kama mikono yangu ingekuwa na nguvu ya kutosha?
Basi kumuinua Amma haingekuwa shida!



Je ingelikuwa aje kama hakungekuwa na chochote kigumu kwa meno yangu?
Unafikiri ningekula vitu aina gani!




Je na kama tumbo langu lingekuwa kubwa kama duara?
Marafiki zangu wote wange nirukia na kucheza cheza juu yangu!



Je ningelikuwa aje na masikio mapana?
Ningelisikia kila kitu, mbali na karibu!



Je ingelikuwa - ninaanza, akaita kwa sauti,
"Shyam, utachelewa, unafikiria kuhusu nini?"



Nikajikuta bado nimesimama na mswaki mkononi,
Nikatabasamu nakuwaza juu ya ile siri yangu ndogo.

